MAHUBIRI N°11: SEMA SASA !

(*Ilihubiriwa juma pili asubuhi 01 desemba 2002 pa Locodjoro, Abidjan - Côte d'Ivoire / www.matth25v6.org*)

Ninazidi kuwaalika muwe na hekima. Musitende zambi moja kama ile ya waisiraeli juu ya manabii, kama waroma juu ya watakatifu. Wanapo nilaani, kuniita pepo, mpinga Kristo, mahubiri nivaquine,… Juweni kwamba ni Mungu munayemtendea hivi. Nilikuwa mpagani tarehe 24 aprili 1993, katika ono moja, nilipata wongofu na kesho baadaye nilipo kuwa nimeketi katika jamaa, nilichukuliwa kwa ono katika nchi iliyokuwa jangwa na nilitumwa kuhubiri hukumu. Ni baada ya maono haya mawili ndipo nilikwenda kanisani kwa mara ya kwanza. Na kama hamuwezi kuchukua Biblia kwa kupinga mambo ninayo hubiri, basi mubaki kimia! Musijibebeshe laana! Sijaingia bado kwenyi seminari wala katika mafunzo fulani ya kibiblia, sisomi vitabu vya maduka zenu vinavyoitwa vya kikristo, kwa maana yeye aliye nituma yuko pamoja nami.

Sasa, nataka kufikia kidogo kusema juu ya Côte d'Ivoire kwa kukamilisha yale nimekwisha kusema: Kwa kuzaliwa kwake, nchi hiyo ni ya aina ya wale wanao zaliwa katika nyumba za wafalme. Mwitu, utajiri udongoni, bahari,… na hiyo ikawaleta nchi jirani kuanguka kifudifudi na kumtumikia katika mashamba zake. Burkina alikuwa mtumwa katika shamba zake na mlinzi wa nyumba yake. Anageuza mafuta ya Nigeria, anatoa umeme mpaka mbali zaidi ya jirani zake. Ndege zote za anga, nyama zote za pori zilikuja kutoka mbali na kupata nafasi yao pembeni yake. Neema, uwezo na utukufu wake ilionekana kama Mungu hakuwa mwenyi haki. Hakika, Mungu alingojea kwake zaidi. Lakini alipokuwa mwenye nguvu, akachagua njia ya waovu, wanao mchukia Mungu na ambao ukumbusho wao unavutwa kila siku kwa volkeno, garika, mvua ngumu, vitisho, tetemeko la nchi, vita,… Zambi inaitwa " mali ya taifa " kwa mfano ya hao wa vaudous, poro, dipri, mask, michezo ya vita, fokué, gbékagnan ambavyo ni mazoezi ya kinyama ambavyo havingetajwa kwa wakati hii ya ukristo. Kila kijiji kina mchawi, mask, mto takatifu, ,…hata kama ni mtu moja tu anaye jitoa kwa mambo kama haya nanyi hamusemi kitu alafu ni kijiji yote inayokuwa katika makosa. Hata ufugo wa nyama za pori ni zambi kwa nchi. Hifazi, ndiyo! Lakini ufugo wa nyama za msitu ni zambi. Tai, simba katika kifungo ni sawa na mtu aliye na kima katika minyororo nyumbani mwake. Ndivyo asema Bwana, muwaache huru na kama sivyo ni laana juu yenu!

Nchi hiyo ilipo pokea Injili tangu karne moja ilipendelea kushika desturi zake za asili. Kati ya mwili, kanzu na Roho ya Yesu, walichagua kanzu na pamoja nayo, laana zote za Biblia. Hakuna hata moja ya laana za Tor.28 ambayo haikuanguka juu yake. Je! Ameshikwa na watu wenyi ukali walio na uso ngumu waliotoka mbali sana? Watu hawa wamekuwa mawe mazito kwa Côte d'Ivoire, wakimusonga katika miji na vijiji vyake vyote? Je! Watu hawa wanatawala juu yake? Ndio, kwa maana utawala wa kweli ni ya uchumi; siasa inakuwa tu na utawala ya heshima. Tunaona pia nyama za pori, nyama ghali ambazo ni wanefili wa kale wanao jaza vijiji kwa nge, joka, nyoka juu ya mkono, masikio yenyi kutobolewa, nywele za uongo na misemwa mpya na wote ni matunda ya zambi. Wamoja wanatoka katika mbegu ya wanyanganyi wanayoitwa "watoto wa mitaani". Ijapo tunajua ya kwamba mitaani siyo mtu kusudi izae watoto. Ni matunda ya uzinifu na ya uchafu, iliyotoka katika ma hoteli, soko, ofisi, magari ndogo ndogo, majengo ambayo hayaja malizwa bado,… Kufanya ngono kabla mali kupewa, ni kwenda kinyume yako binafsi, kinyume ya nchi yako na kinyume ya Mungu. Na dunia imejaa na mambo haya. Makao za chuo kikuu ni mahali pa ukahaba wa hali ya juu. Na mwanamke wa kwanza anawagawia kondomu ili nchi ijichafuwe zaidi, na hivyo anakubali uchafu, uzinifu na ukahaba kisheria. Si lazima kondomu zishauriwe duniani. Na Côte d'Ivoire imedumu katika uchafu hata mchezo kama mapouka ikubaliwe kisheria na kupelekwa katika nchi za kigeni kama kahawa na kakao. Barabara za kiakida, gazeti zinazoonyesha wanawake uchi zinaruhusiwa. Zaïre, nchi hiyo ya machafuko, ni hiyo inatumiwa kama mfano ya kufwata. Mtu anapokataliwa katika nchi yake anaweza kuja kujionyesha hapa. Côte d'Ivoire imeonyesha kwamba kuhusu zambi inaweza kufanya ubaya zaidi kuliko nchi nyingi. Na ni watu wachafu wengine kama Hanny Tchellé, alipo cheza akiwa uchi katika filme nyingi hata hapo hapo anapendelewa kama muburudishaji wa televisheni ili aharibu ujana. Nchi zaifu!

Shetani amefanya dunia kuwa Edeni yake na mwanamke kuwa chombo cha matangazo. Alama moja tu ya kibiblia ya urembo ni uso. "Rebeka [Mwa.24:16], Sara[Mwa.12:11], Rakeli [Mwa.29:17], Abigaili [1 Sam.25:3], Tamari [2 Sam.14:27],... Lakini shetani akafanya alama nyingine: tako, tena kitofu, rangi ya mwili, tena mapambo iliyo uharibifu ya ukamilifu wa umungu: namna ya kusema *"ingemupasa Mungu kufanya namna hii "*. Imetayarishwa kwenu kutendewa kama ilivyo kuwa kwa Yezebeli. Mkono wa uungu ukashikamana na mbwa kwa kula mama mzee wenu ambaye ni Yezebeli lakini kulitokea nini? Mbwa hawakugusa kichwa, miguu, na mikono kwa sababu ya kujipodoa na rangi. Dada zangu, Mungu anapendezwa kuwaona namna alivyo waumba. Mubaki vile vile!

[...] na ni kama yote ile haikutosha, kwa mfano ya manabii wa Baali, alimtia Ahaba na mke wake Yezebeli kwa ufalme. Mwovu zaidi kuliko wana wake wote. Yule aliyempiganisha baba yake Houphouët tangu miaka 1970 pasipo kuchoka na ambaye, kwa mwaka 1990 akainua nyumba kumuasi baba huyo. Sawa sawa na Hamu, akaweka nje uchi ya baba yake machoni mwa dunia na kusukuma nchi yote kufanya hivyo. Na ni ile ile roho ya uasi iliyo sukuma Côte d'Ivoire juu ya Ufaransa. Roho yote ya kupinga Ufaransa ni ya shetani. Ule ule Mungu ambaye hawezi kusukuma Kanisa kupinga Kristo wala mwanamke kumpinga mume, yule Mungu hawezi kufurahishwa na uasi wa Côte d'Ivoire juu ya Ufaransa wala uasi wa Kongo juu ya Ubeljiji. Na munapo tenda hivi, kabla ninyi kupokea vitu mikononi mwao, muwe na unyenyekevu na bidii ya kuwaomba msamaha. Sisemi kwamba Ufaransa haikufanya ubaya lakini ninyi hamuna sheria ya kufanya mambo munayo yafanya. Lakini ni ile ile pepo iliyo ingilia Côte d'Ivoire wakati aliwekwa kwa ufalme. Lakini alipo zuia baba yake kutawala taifa yote, namna gani yeye mwenyewe atatawala juu ya nchi nzima? Je! Alipo tesa kwa fimbo, yeye mwenyewe hataweza kuteswa kwa nge? Kumuweka mtu kama huyu kwa ufalme ni kuita juu ya nchi laana ambayo ingemwangukia yeye peke. Ikiwa kiti chake cha enzi kitasimama imara kwa amani hata yeye kutawala nchi nzima hapo sasa mimi si mtu wa Mungu na Mungu hakusema nami. Mchungaji Daudi akawasihi waamini wake kufanya hiyo uchaguzi lakini Mjuu Sana hakutaka mimi nijichafue na uchaguzi kama huu. Kama Côte d'Ivoire ingepewa uchaguzi kati ya Mungu na Shetani hakika ingechagua Shetani pamoja na makanisa na manabii wake. Mungu anapoleta kiti cha enzi, anakisimamisha imara. Ni kinyume ya nyinyi wenyewe ndipo mulifanya uchaguzi huu. Ninasema mambo haya kufwatana na yale nilipokea toka kwa Mungu. Yeye na mke wake ni watoto wangu na

wizara zao zote ni wajukuu wangu. Lakini kabla niingie kwa watu kama hao kwa wema, inabidi wafukuze hazarani maprezidenti na manabii wote wa makanisa wanao kula mezani mwao na wakate shauri ya kukataa ushirika pamoja nao.

Na hata tunaona mke wake Yezebeli, ambaye alisoma katika chuo kikuu akijiweka kama nabii, akiwaonya wakristo hata kuwasihi wachungaji kutumia kondomu na kuishauri kwa waamini wa makanisa zao, hivyo akaingiza mkono chafu katika vitu vitakatifu, kama ingewezekana. Na hao wachungaji, maprezidenti na manabii wa makanisa, hao mafalme ndogo ndogo hawajaribu hata kidogo kumufungisha kinywa huyo mupagani mdogo aliye pale leo na hatakuweko kesho. Ninyi, CNEPECI, FECI [*shirikisho mbili kubwa kubwa za makanisa za huko Côte d'Ivoire*], ninyi! Sanduku za wachawi wanao vikwa ngozi ya kondoo, Yesu Kristo tayari amewashinda ninyi! Munapenda kula mezani mwa Mungu na pia mezani mwa Kaisari? Upanga utafwatana nanyi mchana kutwa na jehanama itawapokea. Adui wa dunia ni nyinyi! Kwa sababu munatafuta kujenga ufalme wa pesa hapo muna papasa papasa zambi? Mungu atawaharibu!... Ninyi, maGoliata wenyi miguu za udongo, ujumbe huu utawapiga. Ni mateso yenu ambayo imeanza. Nyinyi! Wachawi! Mbwa mwitu za mwili na nono! Nyoka zilizo fugwa! Makao ya Shetani, munalewa kwa damu ya watu wasio na kosa wanao tafuta wokovu, muda gani mutaishi tena duniani? Na kuzimu na ziwa la moto na hadese yote havichoki kulia juu yenu: Hukumu! Hukumu! Hukumu! Kwa nini? kwa sababu nchi yenu ni kuzimu. [sehemu isiyo tangazwa]...

Munaingizana katika mambo ya siasa na munasema: hatufanyi siasa! Ni kama mtu anayesema: *"sile nyama ya nguruwe lakini nakula tu supu ya nguruwe"*.

Kwa mwaka 1993, nchi hiyo iliinuka juu ya wanainchi wa Ghana, watu maskini waliyokuja juu ya nchi iliyo ya kupokea watu ili kutafuta mkate wao. Niliona binadamu wakifa mbali na nchi yao katika hali isiyo hitajika hata kwa nyama. Huko Yopougon, karibu na Saguidiba, mwanamke moja alikufa kwa mtwangiyo iliyo ingizwa katika uchi wake hata tumboni. Kusihi na msamaha gani hakuomba? Rehema gani hakufanya mbele ya hii Côte d'Ivoire iliyo mbovu ambayo leo inakunjamia kila nchi pamoja na masemi [kama] ya mwana kondoo! Kwa nini kwa pato ya kwanza, hospitali ya kwanza ya Côte d'Ivoire baada ya tarehe 19 septemba ilikuwa Ghana? Tangu 1993, hizo damu zisizo na kosa hazikuacha kulilia Mungu: "mpaka siku gani, Mungu mwenye haki na wa kweli, utachelewa kuhukumu na kulipisa kisasi damu yetu juu ya wakaaji wa nchi hii?". Baada ya hayo, Côte d'Ivoire kupitia mwana wake Yodé ilitoa kaseti kwa kusifu maovu yake na nchi nzima ilicheza kwa ile kaseti. Kwenda kinyume ya mgeni, mjane wala yatima, Mungu hawezi kuiacha pasipo malipizi. Na kama ningekuwa askari, singe chukua silaha kwa kupigania nchi kama hiyo, kwa ajili ya Sodomo na Gomora. Sitakubali hata kidogo kufa kama adui ya Mungu. Mimi ni kwanza mkristo kabla ya kuwa mwanainchi wa Côte d'Ivoire. Kila mtu anakufa na taji na maandiko juu ya taji yake, kile ambacho alikishinda maishani mwake… nchi ya tumaini, nchi yenyi kupokea watu, nchi ya undugu wa kweli? Mungu ni upendo lakini yeye pia ni Mungu wa haki na wa hukumu. Mti kila mara huanguka kwa upande inayoegemea !

MAWASILIANO: Ndugu Filipo:+ 225-0252-0252 E-mail: kacou.philippe@yahoo.fr
Upate mahubiri katika site ya: www.matth25v6.org